**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

## KIKAO CHA PILI

**30 JANUARI, 2019**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

______________________

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

## KIKAO CHA PILI – TAREHE 30 JANUARI, 2019

## I. DUA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Maelezo ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuhusu Muswada wa Sheria ya Hali ya Hewa Tanzania wa Mwaka 2018 *[The Tanzania Meteorological Authority Bill, 2018].*

Maelezo ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuhusu Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini wa Mwaka 2018 *[The Land Transport Regulatory Authority Bill, 2018].*

**MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Miundombinu kuhusu Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania wa Mwaka 2018 *[The Tanzania Meteorological Authority Bill, 2018].*

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Miundombinu kuhusu Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini wa Mwaka 2018 *[The Land Transport Regulatory Authority Bill, 2018].*

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuhusu Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania wa Mwaka 2018 *[The Tanzania Meteorological Authority Bill, 2018].*

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuhusu Muswada wa Sheria ya

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini wa Mwaka 2018 *[The Land Transport Regulatory Authority Bill, 2018].*

## III. MASWALI:

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

### 11. MHESHIMIWA ANNE KILANGO MALECELA (KUTEULIWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Barabara ya Hedaru – Vunta – Myamba Wilaya ya Same ni korofi sana na kusababisha usafiri wa barabara ya Tarafa ya Mamba/Vunta kuwa mgumu:-

Je, Serikali inawasaidiaje Wananchi wa Tarafa ya Mamba/Vunta ili waweze kuendelea kiuchumi.

### 12. MHESHIMIWA JOHN WEGESA HECHE (TARIME VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Hospitali ya Wilaya ya Tarime imeelemewa na Wagonjwa kwa sababu inapokea Wagonjwa wengi kutoka Wilaya ya Tarime na Rorya; pamoja na uchache wa Vituo vya Afya, Zahanati na vifaa katika maeneo mengi ya Wilaya hizo:-

Je, ni kwa nini Serikali isipandishe hadhi Hospitali hiyo na kuwa Hospitali ya Mkoa.

**13. MHESHIMIWA ALMAS ATHUMAN MAIGE (TABORA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Serikali imeanzisha Sera nzuri ya Viwanda nchini ili kukuza uchumi wa Viwanda na maendeleo kwa Wananchi:-

(a) Je, Serikali haioni upungufu wa Mafundi Mchundo na Mafundi Sadifu kuwa ni kikwazo cha ufanisi wa Sera ya Viwanda;

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuziimarisha Shule za Ufundi za Moshi, Ifunda, Tanga na Mtwara ili kuwaandaa na kuwapatia Mafundi Sadifu kufanikisha Sera ya Viwanda nchini.

## WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

**14. MHESHIMIWA HAMIDA MOHAMED ABDALLAH (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Kilwa ni moja kati ya Miji Mikongwe katika Afrika Mashariki tangu 900 – 1700 AD ikiwemo na Lamu, Mombasa, Sofala na

Zanzibar; Miji hii ilipewa heshima ya jina la Urithi wa Dunia *(World Heritage Sights)* na husaidiwa na Mataifa mbalimbali kama Marekani, Japan, Ujerumani, Uingereza na Taasisi ya UNICEF:-

Je, Serikali ya Tanzania inafaidika na nini kutoka kwenye Mataifa hayo yanayosaidia nchi zenye Miji ya Urithi wa Dunia.

**15. MHESHIMIWA VEDASTO EDGAR NGOMBALE (KILWA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Hifadhi ya akiba ya Selous imekuwa ikihamisha alama za mipaka na kuchukua eneo la ardhi ya Vijiji katika Jimbo la Kilwa Kaskazini bila ya kushirikisha Serikali ya Vijiji:-

Je, Serikali iko tayari kusimamia Mamlaka ya Hifadhi hiyo kurudisha alama za mipaka katika maeneo ya awali ili kuepusha mgogoro unaoweza kutokea.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**16. MHESHIMIWA JOSEPH OSMUND MBILINYI (MBEYA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Katika bajeti ya mwaka 2017/2018 Wizara ya Afya iliomba na kutengewa Shilingi bilioni 5 kwa ajili ya ukamilishaji wa jengo la maabara na ununuzi wa vipimo vya kisasa kama CT Scan na MRI Scan katika Hospitali ya Rufaa ya Mbeya:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kimeshatolewa mpaka sasa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi huo;

(b) Kwa kuwa bajeti inayohitajika imeshatengwa; Je, ni lini ujenzi huo utakamilika.

**17. MHESHIMIWA AYSHAROSE NDOGHOLI MATEMBE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Tatizo la Watoto wanaoishi kwenye mazingira hatarishi linazidi kuwa janga la kitaifa nchini huku jitihada za kulikabili zikionekana kutopewa kipaumbele hali ni mbaya katika Majiji makubwa kama Dar es Salaam, Mwanza na Mbeya ambapo idadi kubwa ya Watoto hao hujihusisha na kuomba pamoja na matukio ya

uhalifu ikiwemo wizi wa vifaa vya magari kwenye maegesho:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha kampeni ya Kitaifa ya kukabiliana na tatizo hili kwa nchi nzima ikiwemo kuwaweka kwenye vituo maalum na kuwapatia huduma za msingi;

(b) Je, Serikali inatambua idadi kamili ya Watoto wanaoishi kwenye mazingira hatarishi kwa nchi nzima.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**18. MHESHIMIWA EDWIN MGANTE SANNDA (KONDOA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Halmashauri ya Mji wa Kondoa imepata eneo la iliyokuwa kambi ya ujenzi wa barabara ya Mela-Bonga pale Kolo kwa ajili ya uanzishwaji wa Chuo cha VETA:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza azma hiyo.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

### 19. MHESHIMIWA MWATUMU DAU HAJI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Kuna baadhi ya Askari Polisi hupandishwa vyeo lakini hawapati stahili zao kama inavyotakiwa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia Askari hao stahili zao.

### 20. MHESHIMIWA ANNA RICHARD LUPEMBE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itajenga Gereza Wilaya ya Mlele.

## WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

**21. MHESHIMIWA TIMOTHEO PAUL MNZAVA (KOROGWE VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 Wananchi wa Korogwe waliahidiwa ujenzi wa barabara ya lami kutoka Korogwe – Dindini hadi Bumbuli:-

Je, ni lini ujenzi huo utaanza.

**22. MHESHIMIWA ISSA ALI MANGUNGU (MBAGALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

(a) Je, barabara ya Kilwa imeshakabidhiwa kwa Serikali kutoka kwa Mkandarasi aliyejenga barabara hiyo (KAJIMA);

(b) Je, Barabara hiyo ipo katika kiwango kinachotakiwa;

(c) Je, ni nani anagharamia ukarabati usiokwisha wa barabara hiyo kati ya Serikali na Mkandarasi.

## WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

### 23. MHESHIMIWA JOHN JOHN MNYIKA (KIBAMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:- Ili kuharakisha upimaji na urasimishaji wa ardhi na makazi, Serikali iliruhusu Kampuni binafsi kufanya kazi hiyo katika maeneo mbalimbali:-

(a) Je, ni lini Kampuni zinazofanya kazi hiyo zitatoa Hati za ardhi au Leseni za makazi kwa Wananchi;

(b) Je, ni vikwazo gani vinakabili zoezi hilo na Serikali inachukua hatua gani kuviondoa ili kuzisaidia Kampuni hizo kumaliza kazi hiyo kwa haraka;

(c) Je, ni lini Serikali itakamilisha mpango Kabambe (*MasterPlan*) mpya wa Jiji la Dar es Salaam ili uwe dira katika upangaji, upimaji na urasimishaji.

## WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

**24. MHESHIMIWA KHADIJA NASSIR ALI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:- Serikali imekuwa ikijitahidi kuvisimamia na kuviwezesha Viwanda vyetu vya ndani lakini cha kusikitisha ni kwamba Serikali imeshindwa kusimamia bidhaa zetu ndani ya soko hili huria. Mathalani, bidhaa za "viua dudu" zinazozalishwa na Kiwanda kilichopo Kibaha bado hazipo sokoni na Wananchi hawana uelewa nazo:-

Je, Serikali haioni kwamba kuendelea kuwekeza fedha kwenye Viwanda vyetu bila ya kuwa na mikakati mizuri ya kibiashara ni kuendelea kutumia vibaya fedha za walipa kodi.

## WIZARA YA NISHATI:

**25. MHESHIMIWA AUGUSTINO MANYANDA MASELE (MBOGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Serikali iliahidi kuanza utekelezaji wa mradi wa umeme wa ujazo (*Densification)* Mkoani Geita

kuanzia mwezi Oktoba, 2018 lakini hadi sasa mradi huo haujaanza:-

Je, ni lini mradi huo utaanza kutekelezwa katika Wilaya ya Mbogwe.

## IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

*(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)*

Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania *[The Tanzania Meteorological Authority Bill, 2018].*

Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini wa Mwaka 2018 *[The Land Transport Regulatory Authority Bill, 2018].*

**DODOMA** — **S. KAGAIGAI**
**30 JANUARI, 2019** — **KATIBU WA BUNGE**